

**HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. FADHILI E. NKURLU KAIMU
MKUU WA MKOA WA SHINYANGA KWENYE UFUNGUZI WA
WIKI YA MAHAKAMA TAREHE 04/02/2017**

Mhe. Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu , Kanda ya Shinyanga R.M. Kibella

Mhe. Jaji Mahakama Kuu , Kanda ya Shinyanga V.L. Makani

Naibu Msajili, Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga Sekele Mwaiseje

Mtendaji, Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga Ernest Masanja

Waheshimiwa Mahakimu ngazi mbalimbali

Watumishi wa Mahakama ngazi mbalimbali

Ndugu Waandishi wa Habari

Ndugu Wananchi mlionhudhuria hapa, Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetuwezesha kukutana hapa. Aidha napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliowezesha kufanyika kwa shughuli hii ya uzinduzi wa wiki ya Mahakama Mkoani Shinyanga.

Tupo hapa leo kufanya uzinduzi wa wiki ya Mahakama, ambapo kauli mbili ni **“UMUHIMU WA UTOAJI HAKI KWA WAKATI KUWEZESHA UKUAJI WA UCHUMI.**

Yapo mabadiliko makubwa yaliyopatikana katika siku za hivi karibuni kutokana na mahakama kuendelea kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa utoaji haki kwa umma tofauti na ilivyokuwa zamani.

Mabadiliko hayo yamefikiwa baada ya kuwepo viashiria kadhaa ikiwemo kupungua kwa malalamiko, mwamko wa umma kuongezeka ambapo idadi kubwa ya wananchi sasa wanaenda mahakamani kutafuta haki zao badala ya kujichukulia sheria mkononi.

Maadhimisho ya wiki ya Sheria

Tukio hili linaashiria kuanza rasmi kwa shughuli za mahakama kwenye mwaka husika na katika kuifanikisha tayari mahakama imeanza kuratibu utoaji wa elimu ya haki na sheria kwa umma ambapo mada mbalimbali huwasilishwa kupitia Radio na madawati maalum ya ushauri yaliyopo kwenye viwanja vya mahakama zote zilizopo kanda hii ili kuwapa fursa wananchi kushauriwa, kufahamishwa haki zao na kuelekezwa namna ya kuzidai kwa wakati ili kuharakisha maendeleo.

Mahakama baada ya kutekeleza maboresho katika utendaji wake wa kila siku hupokea mrejesho wa mara kwa mara kutoka kwa jamii na tumeona yapo mabadiliko makubwa katika miaka ya hivi karibuni ambapo wananchi wanaonesha mwamko wa kutafuta haki zao mahakamani tofauti na zamani.

Aidha, kuongezeka mahakamani kwa idadi ya kesi za jinai, mirathi na madai ni miongoni mwa viashiria vinavyothibitisha mafanikio hayo kutokana na mwendelezo wa mpango wa utoaji wa elimu ya haki na sheria kwa umma unaoratibiwa na Mahakama kwa kushirikiana na wadau wake kila mwaka.

Kesi nyingi hivi sasa hazichukui muda mrefu wa kusikilizwa kwa sababu mmejiwekea lengo maalum kwamba ndani ya siku 90 uamuzi uwe umetolewa, kutokana na maboresho hayo imefikia wakati sasa baadhi ya Mawakili wanalamika kuhusu kasi hii mnayoenda nayo lakini hatuna namna ni lazima haki ipatikane kwa wakati ili kuwezesha ukuaji wa uchumi wa jamii na Taifa kwa jumla.

Maadhimisho ya Wiki ya Elimu ya Sheria ikiwa ni sehemu ya sherehe za kuelekea maadhimisho ya kilele cha Siku ya Sheria nchini ambapo pia katika mikoa yote ya Tanzania wananchi wataweza kupata fursa ya kujua sheria katika sehemu maalum zitakazokuwa zimeandaliwa.

Mahakama itawaelimisha wananchi jitihada mbalimbali ilizochukua zenye lengo la kuboresha huduma zake kuitia mpango-mkakati wa miaka mitano inaoutekeleza katika kutoa haki kwa wakati na kuwezesha ukuaji wa uchumi. Haya yatafanyika kwenye mabanda yatakayokuwepo kwenye Viwanja vya jeshi la zimamoto na uokoaji kabla ya kilele chake.

Napenda kutoa rai kwa wananchi kutembelea sehemu zote zilizoandaliwa kwa ajili ya utoaji elimu ya sheria nchini kwa ajili ya kujifunza mambo mbalimbali na kupata huduma za kisheria

Miongoni mwa huduma zitakazotolewa katika wiki hii ya Mahakama ni pamoja na taratibu za ufunguaji mashauri katika ngazi mbalimbali za mahakama, taratibu za kesi za dhamana, taratibu za rufaa, taratibu za

kesi za mirathi, ndoa na talaka, taratibu za kupokea na kushughulikia malalamiko na msaada wa kisheria.

Licha ya mafanikio yaliyopatikana katika mhimili huu muhimu wa mahakama, bado zipo changamoto mbalimbali ikiwemo kwa baadhi ya mahakimu wasiojali weledi wa taaluma yao kujihusisha na vitendo vya rushwa kitu ambacho kinapelekea watu kushindwa kupata haki na kuchafua sifa njema ya mhimili muhimu wa dola wa mahakama. Nitumie fursa hii kuwataka Waheshimiwa Mahakimu kuzingatia misingi ya maadili ya taaluma yenu ili muweze kutoa haki kwa wananchi.

Baada ya kusema hayo natamka kuwa nimezindua rasmi wiki ya Mahakama.

“Asanteni kwa kunisikiliza”